

**HOTUBA YA MGENI RASMI KATIBU MKUU -MAENDELEO YA  
JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO WAKATI AKIFUNGA  
MAFUNZO YA MAJARIBIO YA MWONGOZO WA KUHAMASISHA  
WANAWAKE KUANZISHA NA KUJIUNGA NA VIKUNDI VYA  
KIUCHUMI KATIKA HALMASHAURI YA MVOMERO  
TAREHE 6 OKTOBA, 2017 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA  
MKUU WA WILAYA**

**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mvomero;**

**Wawezeshaji kutoka Wizarani, CARE International na VICOBA  
Endelevu;**

**Ndugu washiriki;**

**Mabibi na Mabwana!**

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya njema na kutuwezesha kuhitimu mafunzo ya majaribio ya mwongozo wa kuhamasisha wanawake kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi. Nimefahamishwa kuwa katika siku tatu za mafunzo mmepata fursa ya kuupitia na kuufahamu mwongozo sambamba na kupata maarifa kuhusu Mfumo wa Hisa na VICOBA. Nawapongeza sana kwa kujitoa kwenu kwa kuwa mmeacha majukumu mengi na kutoa kipaumbele kwa kazi hii.

**Ndugu washiriki;** Kwa namna ya pekee, naushukuru Uongozi wa mkoa, wilaya na Halmashauri kwa kutuhifadhi mahali hapa na kutuhakikisha ulinzi na usalama wetu. Aidha, natumia fursa hii kulishukuru shirika la Kimataifa la Care kwa kukubali kufanya kazi kwa ubia na Wizara ili kufanikisha zoezi hili. Vile vile, nalishukuru shirika la VICOBA ENDELEVU kwa kushiriki katika kutoa uelewa kuhusu VICOBA.

**Ndugu washiriki;** Mwongozo wa Kuhamasisha Wanawake Kuanzisha na Kujiunga na Vikundi vya Kiuchumi ni moja ya jitihada za utekelezaji wa Sera ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017-2022), Mpango wa Taifa wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 – 2020/21) na Ilani ya Uchanguzi ya CCM ya mwaka 2015.

**Ndugu washiriki;** Ni matumaini yangu kuwa mwongozo huu utasaidia siyo tu kuboresha jitihada za kuhamasisha wanawake kujiunga na Vikundi vya Kiuchumi bali pia utawezesha kuwa na takwimu na taarifa sahihi za vikundi kwa ajili ya kuchambuzi na kujenga hoja kuhusu maamuzi mbalimbali. Hivyo ni jukumu la kila mmoja wetu aliyeshiriki katika mafunzo haya kuhakikisha mwongozo huu unatekelezwa ipasavyo na kuleta matokeo yaliyotarajiwa ya kuwawezesha wanawake kiuchumi ikiwemo kuboresha hali ya maisha yao.

**Ndugu washiriki;** Hii ni fursa kwenu kubeba mbinu mlizopata katika mafunzo haya ili mkazitumie kwa kufuata mwongozo huu kuhamasisha wanawake kuanzisha/kuunda au kujiunga na vikundi vya kiuchumi ikiwemo VSLA, SILC, VICOBA na SACCOS. Katika uhamasishaji wanawake kujiunga na vikundi vya kiuchumi mnatarajiwa kuhakikisha yafuatayo yanafikiwa:

- (i) Wanawake wanaelewa dhana ya kuweka akiba na kupata mikopo na mchango wake katika kupambana na umaskini;

- (ii) Wanawake wanajiunga na kuanzisha vikundi vya aina mbalimbali kulingana na mazingira yao na kutokana na uchaguzi wao.
- (iii) Vikundi vya kiuchumi vilivyopo na vinavyoanzishwa katika maeneo yenu vinakuwa endelevu na kuwanufaisha wanawake kiuchumi na kijamii.
- (iv) Kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu vikundi vilivyoanzishwa, maendeleo ya vikundi hivyo na faida za kiuchumi na kijamii wanazopata wanawake kwa takwimu na ushahidi.
- (v) Kujenga Ubia na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa mwongozo huu na kutambua mchango wao .

**Ndugu washiriki;** Nimefahamishwa kuwa wakati wa mafunzo mmeainisha mambo na changamoto mbalimbali zinazohitaji kufanyiwa kazi ikiwemo uratibu mbovu unaosababisha Halmashauri na Kata kutokuwa na taariifa sahihi za vikundi na viwango vya ada ya usajili wa vikundi vilivyowekwa na mwongozo wa usajili wa vikundi kutofautiana na viwango vya usajili vilivyowekwa na madiwani. Nawaahidi kuzifanyia kazi changamoto zote zinazo katika ngazi ya Taifa kwa kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Nachukua fursa hii pia kuwataka kutatu changamoto zinazo ndani ya mamlaka na uwezo wa Halmashauri na Mkoa. Nawataka pia kuhakikisha Mpango Kazi mliojiwekea unatekelezwa ipasavyo na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kuzingatia Muundo mliokubaliana.

**Ndugu washiriki;** kabla ya kumaliza hotuba yangu, naomba kuwakumbusha washiriki kuwa ni Halmashauri ya Mvomero na Halmashauri ya Rombo pekee ndizo zimepata bahati hii ya kufanyiwa

majaribio, hivyo ni muhimu mkatumia kikamilifu fursa hii kwa manufaa ya halmashauri yenu na taifa kwa ujumla.

**Ndugu washiriki; baada ya kusema hayo natamka kuwa mafunzo kwa ajili ya majaribio ya Mwongozo wa Kuhamasisha wanawake kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi yamefungwa rasmi!**

#### **ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**